# UHUSIANO KATI YA SERIKALI ZA MITAA NA SERIKALI KUU

## Utangulizi:

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, "Serikali za Mitaa" maana yake ni vyombo vya Kiserikali vilivyoundwa kwa mujibu wa ibara ya 145 ya Katiba hiyo kwa madhumuni ya kutekeleza madaraka ya umma. Vyombo vya Kiserikali vilivyoundwa na sheria kufuatia maelekezo hayo ya Katiba ni Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Majiji/Halmashauri za Vijiji. Kimsingi majukumu ya mamlaka za Serikali za Mitaa ni kama yalivyoainishwa katika Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa, ambayo ni kuhusu mahusiano ya vyombo hivi na Serikali Kuu. Sheria za Serikali za Mitaa na sheria nyingine za nchi zinaeleza kwa undani zaidi majukumu na mipaka ya Serikali za Mitaa na vyombo mbalimbali vya Serikali Kuu ili kuondoa mwingiliano. Kwa hiyo, mahusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu yanatawaliwa na sheria, na kamwe hayategemei maelewano kati ya viongozi na watumishi wa umma walio katika Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

## Maana na Nafasi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika Utawala na Uongozi wa Nchi

Kwa mujibu wa Ibara ya 6 na Ibara ya 151 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania neno "Serikali" maana yake ni pamoja na Serikali ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Halmashauri ya Wilaya au ya Mji; na pia mtu yeyote anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali au Halmashauri. Serikali za Mitaa ni vyombo vya Kiserikali vilivyoundwa kwa mujibu wa Ibara ya 145 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa madhumuni ya kutekeleza madaraka kwa umma.

Serikali Kuu ni chombo chenye mamlaka na madaraka katika nchi nzima kwa mujibu wa Katiba na Sheria mbalimbali zilizotungwa na Bunge. Serikali za Mitaa ni vyombo vyenye mamlaka na madaraka katika eneo husika la Tanzania ambavyo vinashughulikia masuala yaliyoainishwa katika Katiba na Sheria zinazoviunda.

Ingawa chimbuko la Serikali hizi mbili ni Katiba ileile, lakini kazi na majukumu yao yanatofautiana katika upana wa maeneo ya utekelezaji na uwajibikaji. Katika majukumu yaliyo mengi, kazi za vyombo hivi viwili ni ya kukamilishana (complementary) au tuseme ya ubia.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi yenye serikali moja. Ingawa ndani yake zimo serikali za mitaa nyingi sana (zaidi ya 10,000), ili kuhifadhi utaifa katika nchi moja, Katiba na Sheria za nchi yetu zimeweka wazi kwamba Serikali Kuu ndiyo kiongozi wa nchi na hivyo Serikali za Mitaa zinatakiwa kuzingatia Sera, Sheria na Kanuni za kitaifa katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali za Mitaa.

**Mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa:**

Sera ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa ya 1998 inaelekeza kwamba mahusiano baina ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu yatatawaliwa na sheria. Aidha, mahusiano yataegemea zaidi katika mashauriano, majadiliano na maelewano badala ya kuegemea katika kutoa, kupokea na kutekeleza amri kama ilivyokuwa siku za nyuma. Kutokana na msimamo huo wa Sera, Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 na 8 za 1982 (Vifungu 174A na 54A kwa mfuatano) zimeelekeza wazi jinsi mahusiano kati ya vyombo hivyo yanavyopaswa kuwa kwa kutaja majukumu ya Serikali Kuu mintarafu uwezo na kazi za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:

(a) Kuzisaidia Serikali za Mitaa kutumia uwezo ziliopewa na kutekeleza kazi zilizopewa kisheria katika hali inayotambua uhuru (wa kufanya maamuzi) ambao Serikali za Mitaa zimepewa;

(b) Kutunga sera za kitaifa na mfumo wa udhibiti kwa ajili ya Mfumo wa Serikali za Mitaa;

(c) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa Serikali za Mitaa ili kuona iwapo zinazingatia sera za kitaifa, miongozo na viwango vya utoaji huduma vilivyowekwa kitaifa;

(d) Kutunga sera na kuweka mfumo wa udhibiti ili kuhakikisha Serikali za Mitaa zinaongoza mawakala wengine wa maendeleo katika maeneo yao katika utekelezaji sahihi wa sera hizo;

(e) Kutoa msaada wa kitaalamu unaohitajika kwa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuendeleza sekta husika za serikali hizo za mitaa;

(f) Kusaidia katika kazi ya utekelezaji wa maamuzi ya Serikali za Mitaa ambayo yanaathiri maendeleo ya sekta husika. Pia Serikali Kuu itapaswa kutambua na kuendeleza jukumu la Serikali za Mitaa katika kutoa huduma na kusimamia shughuli za maendeleo katika maeneo yao.

**Viongozi na Vyombo vya Serikali Kuu vyenye Mahusiano ya karibu na Serikali za Mitaa**

**(a) Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa**

Waziri amepewa majukumu kadhaa mintarafu Serikali za Mitaa k.m.

(i) kukuza/kuanzisha Serikali za Mitaa na kuhakikisha zinaendelea na zinashirikisha umma katika kufanya maamuzi juu ya masuala yanayogusa maisha yao;

(ii) kujitahidi kuhakikisha Serikali za Mitaa zina rasilimali na watumishi wenye mafunzo na stadi ili kujenga Mfumo wa Serikali za Mitaa wenye nguvu katika utoaji huduma;

(iii) Kujitahidi kuhakikisha Serikali za Mitaa zina uhuru katika uendeshaji wa mambo yao;

(iv) Kuhakikisha Serikali za Mitaa zinawajibika kwa wananchi na kwa jumla zinasaidiwa ili kuimarisha uwezo wao wa kutoa huduma;

(v) Kuanzisha Halmashauri za Wilaya/Miji;

(vi) Kutoa kibali kwa Msajili wa Vijiji kuandikisha eneo liwe Kijiji;

(vii) Kuweka vigezo vya mamlaka ya mji mdogo kuwa Halmashauri ya mji;

(viii) Kuondoa kizuizi ili shughuli za Halmashauri ziweze kufanyika pale ambapo wajumbe wengi katika kikao cha Halmashauri wana maslahi katika suala linalojadiliwa na hivyo maamuzi kutoweza kufanywa;

(ix) Kuzitangazia Serikali za Mitaa masuala ambayo ni jukumu la Serikali Kuu au la ngazi nyingine za Serikali za Mitaa tu ili zisiyashughulikie au kuyaingilia;

(x) Kuidhinisha sheria ndogo za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji;

(xi) Kuidhinisha Kanuni za Kudumu za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa na Majiji na marekebisho ya Kanuni hizo;

(xii) Kutunga Kanuni za Fedha;

(xiii) Kutunga sheria ndogo zinazofanana zitakazotumiwa na Halmashauri za Wilaya au za Miji au Mamlaka za Miji Midogo au Vijiji au kikundi cha Halmashauri za aina fulani (kati ya hizo zilizotajwa);

(xiv) Kuchukua hatua zinazofaa kulazimisha Halmashauri kutekeleza kazi au majukumu yake;

(xv) Kutoa uamuzi ambao utakuwa wa mwisho iwapo Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya/Mji ametuhumiwa na Madiwani na akakata rufaa kwa Waziri;

(xvi) Kuhamishia kwa mtu au kikundi cha watu wengine kazi fulani au kazi zote za Halmashauri baada ya kufanya uchunguzi na kugundua kuwa Halmashauri husika haina uwezo wa kiutekelezaji wa majukumu yake;

(xvii) Kuvunja Halmashauri inayoshindwa kutekeleza sheria au inayoendesha mambo yake kinyume na sheria;

(xviii) Kuteua Wakurugenzi wote isipokuwa wale wa Majiji;

(xix) Waziri ni mamlaka ya uteuzi, kuthibitisha kazini na nidhamu kwa Wakurugenzi wote isipokuwa wa Jiji;

(xx) Kutunga Kanuni za Maadili ya Madiwani.

## (b) Mkuu wa Mkoa

Majukumu ya Mkuu wa Mkoa mintarafu Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria za Serikali za Mitaa na Sheria ya Tawala za Mikoa Na. 19 ya 1997 ni kama yafuatavyo:

(i) Kuhakikisha panapatikana utulivu na amani katika Mkoa;
(ii) Kuidhinisha sheria ndogo za Mamlaka za Miji Midogo;
(iii) Kuchunguza uhalali wa matendo au maamuzi ya Serikali za Mitaa katika Mkoa wake iwapo yametiliwa mashaka na kuchukua hatua ifaayo au kumjulisha Waziri;
(iv) Kutoa idhini kwa mtu yeyote kimaandishi kukagua vitabu vyote vya hesabu vya Halmashauri na kumbukumbu za Halmashauri;
(v) Kuelekeza Serikali za Mitaa namna ya kutangaza mizania ya hesabu zake na taarifa yoyote iliyotolewa na Mkaguzi wa nje juu ya hesabu za mwaka za Halmashauri;
(vi) Kuelekeza nguvu iwekwe wapi katika utekelezaji wa sera za Serikali;
(vii) Kuwezesha na kusaidia mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo katika Mkoa wake kwa kuweka mazingira mazuri ya kuziwezesha kutekeleza kazi na majukumu yao;
(viii) Kwa kupitia Kamati ya Ushauri ya Mkoa, kutoa ushauri kwa Serikali za Mitaa kuhusu mipango yao ya maendeleo;
(ix) Kupokea mihtasari ya Halmashauri kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

**(c) Sekretarieti ya Mkoa**

Majukumu ya Sekretarieti ya Mkoa kuhusiana na Serikali za Mitaa za ngazi ya Wilaya ni haya yafuatayo:

(i) Kupitia bajeti ya Halmashauri na kutoa ushauri kuhusu sera za Taifa, mipango ya kitaifa na Kanuni za Fedha kwa kila Mkurugenzi wa Halmashauri ili masuala hayo yazingatiwe katika bajeti za Halmashauri;
(ii) Kuunganisha mipango na bajeti za Halmashauri zilizo katika Mkoa na kuziwasilisha kwenye ngazi ya kitaifa ili zijadiliwe na kutolewa fedha;
(iii) Kuchambua na kuunganisha bajeti za Halmashauri za robo mwaka za utekelezaji wa mipango na matumizi ya fedha na kuziwasilisha kwenye Wizara yenye Dhamana ya Serikali za Mitaa pamoja na maoni ya Sekretarieti ya Mkoa;

(iv) Kufuatilia na kutathmini matumizi ya ruzuku ya Serikali za Mitaa zilizo katika Mkoa.

**(d) Mkuu wa Wilaya**

Majukumu ya Mkuu wa Wilaya kuhusiana na Serikali za Mitaa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuhakikisha kuwa kuna utulivu na amani katika Wilaya;

(ii) Kuziwezesha na kuzisaidia Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwa kuweka mazingira mazuri ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza kazi na majukumu yao;

(iii) Kuhakikisha watu wote na mamlaka zote zinatekeleza maamuzi, miongozo na Kanuni za Serikali mintarafu ukuzaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa;

(iv) Kuchunguza uhalali wa matendo au maamuzi ya Serikali za Mitaa zilizo katika Wilaya yake iwapo yametiliwa mashaka na kuchukua hatua ifaayo au kumjulisha Waziri;

(v) Kupokea mihtasari ya Halmashauri kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri;

(vi) Kumwagiza kimaandishi mtumishi yeyote wa Halmashauri aliye katika vazi rasmi kumkamata mtu anayevunja sheria ndogo ya Halmashauri mbele yake.

**(e) Katibu Tarafa**

Katibu Tarafa ana jukumu la:

– Kuhakikisha sheria ndogo za Halmashauri zinatekelezwa katika eneo la Tarafa yake, na pia kama Mlinzi wa Amani katika tarafa yake, atakuwa na mahusiano ya karibu na Maafisa Watendaji wa Vijiji na wa Kata ndani ya Tarafa yake.

**Mwisho:**

Suala la mahusiano ni muhimu sana kwa sababu kila mmoja anapojua barabara majukumu yake na mipaka ya majukumu hayo, nafasi za kuingiliana hupungua au kutoweka kabisa; ushirikiano huongezeka na mafanikio ya kazi za Halmashauri huwa makubwa.

Ingefaa ieleweke kuwa Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa, ndiye anayewajibika kisiasa katika Bunge kuhusu maendeleo na ufanisi wa Serikali za Mitaa. Hivyo ni wajibu wake kuziongoza, kuzisaidia na kuziwezesha Halmashauri ili zitekeleze majukumu yao kwa mujibu wa Katiba, Sera na Sheria za nchi.